
# EIA FOR MILLING FACTORY AT FINYA SHEHIA, WETE DISTRICT








**[Final Report]**


**Submitted for approval to:**

*Zanzibar Environmental Management Authority*

*P.O. Box 2808, Zanzibar*

*Tel: +255 24 2239007 Fax: +255 24 2234606*

*Email:zemaznz@gmail.com/ zemaznz@yahoo.com*

**Consultant:**

*ISMACO Company*

*P.O. Box 291, Chake Chake*

*Tel:+255 715 667 531*


**[August, 2023]**

# SWAHILI SUMMARY


Kampuni ya FLYING FOX ni kampuni yenye uzoefu katika biashara ya uzalishaji wa bidhaa mbalil mbali zitokanazo na unga wa ngano ikiwemo mikate boflo, mandazi, etc pamoja na shughuli jengine za kibiashara. Kampuni nia ya kuekeza kiwanda cha kusaga nafaka (ngano na mahindi) na kuzalisha unga wa ngano na sembe katika Shihia ya Finya, wilaya ya Wete Pemba. Kimsingi malengo na matarajio ya mradi huu unaenda sambamba na malengo na mikakati ya serikali ya Wilaya na serikali kuu katika uekezaji hasa eneo la Viwanda. Hadi sasa Pemba haina aina ya mradi kama huu ukilinganisha na Unguja, hivyo kusababisha unga wa ngano na wa sembe kuagizwa nje ya kisiwa cha Pemba. Kuwepo kwa kiwanda kusaga nafaka katika eneo la Finya kitapunguza umbali na pia kitaongeza upatikanaji wa huduma ya unga safi na salama.

Kama ilivyoelekeza sheria ya Zanzibar ya Mazingira nambari 3 ya mwaka 2015 kwamba, shughuli yoyote ya kimaendeleo / mradi ambayo inatarajiwa kufanyika katika eneo lolote na kupelakea mazingira kubadilika, ni lazima mradi huo ufanyiwe ripoti ya kimazingira na kupatiwa cheti cha kimazingira kabla ya kuanza utekelezaji. Kwa maana hio mradi huu uko katika hatua hio ya kisheria na kutaraji kupata cheti kutoka kwa mamlaka husika (ZEMA). Sheria na kanuni zinazohusiana na mradi huu zimeangaliwa na kupitiwa kwa makini ili kuweza kuboresha na kufuata taratibu kwa ufanisi mzuri na mahusiano mazuri kwa serikali na wadau wengine.

Mradi pendekezwa unatarajiwa kuwekezwa katika Shehia ya Finya, wilaya ya Wete kwenye eneo lenye ukubwa wa 10,000 sqm (1 h) pembazoni kidogo mwa barabara ya Finya – Wingwi. Eneo haliko mbali sana na makaazi ya watu na karibu na mji wa kibiashara wa Wete mjini. Pia eneo lina miti, nyasi na mazao ya mda mfupi yanayoweza kuhamishika ikiwemo mohogo, viazi vitamu, migomba na minazi. Eneo lina muinuko mdogo usiosumbua kwa ujenzi wa kiwanda na linapokea mvua ya wastani. Hapana miundombinu ya kusafirishia maji ya mvua ya uhakika na inategemea zaidi michrizi/misingi ya asili pembezoni na katikati ya enao na michirizi ya muda.

Mradi pendekezwa wa kusaga nafaka na mahindi na ngano utakua na sehemu kuu tatu za ujenzi: (i) usafishaji wa awali wa kiwanja ukijumuisha kulipa fidia ya mazao, kuondosha miti, kuchimba na kuweka sawa eneo. (ii) Sehemu nyengine ni upimaji wa foundation na

kugawanya maeneo muhimu ya kiwanda ikiwemo kisima na matanki ya kuifadhia maji, mashine za kusafisha na kuzalisha unga, umeme, bomba za maji, mapaa, sehemu ya kugeshea magari, na n.k. Pia kutakua na ujenzi wa miundombinu ya maji taka na maji safi, taka ngumu na sehamu za kuhifadhia chemicali na mafuta machafu. (iii) Kipindi cha uendeshaji kutakua na utoaji wa huduma ya kuuza unga wa ngano na sembe pamoja na uzingatiaji wa usalama wa kiwanda na watu kutokana na moto, wizi na majanga mengineyo.

Matayarisho na uendeshaji wa kiwanda kuna athari nyingi za kimazingira zitakazojitokeza katika kipindi cha ujenzi na uenedeshaji lakini hazitokua kubwa na nyingi sio endelevu, pia mpango wa kudhibi adhari hizo umeainishwa katika ripoti hii ya kimazingira na taasisi ambazo zitahitajika kusimamia zimeainishwa katika kila tukio linalotazamiwa kutokea. Hata hivyo, inaonyesha wazi kwamba mradi huu utakua na faida kubwa kwa jamii na serikali za kiuchumi na za kuhuduma. Lakini kunahitajika mashirikiano baina ya muekezaji na wadua wanaozunguka eneo la maradi. Matatizo mengi ya kimazingira na kijamii ya mradi huu yanaweza kutatulika kwa muda mfupi na sio matatizo endelevu.

Kuepo kwa mradi katika eneo lilopendekezwa kutakua na faida zaidi na ni sehemu salama kwa uekezaji wa kiwanda cha unga ikizingatiwa tatizo la uhaba wa viwanda vya aina hii katika wilaya ya Wete na Pemba kwa ujumla, Pia urahisi wa kusafirisha unga wa ngano na sembe safi na salama vijijini na mjini.